

Joyce anaona namba


Hanrie Coetzee
Laura de Lange
Arthur Attwell





Kitabu hiki ni mali ya







bookdash.org

A TECEC project, funded by Theirworld



Joyce anaona namba

(Zanele sees numbers)

Illustrated by Hanrie Coetzee

Written by Laura de Lange

Designed by Arthur Attwell

Edited by Catherine Deiner

Translated by Aziza Abdullah Ngume

with the help of the Book Dash participants in Grahamstown on 12 November 2016.

Typeset in Crimson and Josefin Sans

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 Licence
(<http://creativecommons.org/licenses/by/4.0/>).

You are free to share (copy and redistribute the material in any medium or format) and adapt (remix, transform, and build upon the material) this work for any purpose, even commercially. The licensor cannot revoke these freedoms as long as you follow the following license terms:

You must give appropriate credit, provide a link to the license, and indicate if changes were made. You may do so in any reasonable manner, but not in any way that suggests the licensor endorses you or your use. No additional restrictions: You may not apply legal terms or technological measures that legally restrict others from doing anything the license permits.

Joyce anaona namba

Hanrie Coetzee • Laura de Lange • Arthur Attwell



Kila mtu anamwambia Joyce kwamba
amezungukwa na namba kila sehemu.
Lakini kila anavyojaribu kutafuta namba
hizo bado hazioni.



Joyce anamwomba Bibi amsaidie
aweze kuona baadhi ya namba.
Bibi anaelekeza kidole kwenye
mitungi iliyoko juu ya rafu na
kuhesabu, “moja, mbili, tatu, nne.”







Lakini Joyce hana furaha.
“Hizo si namba. Hiyo ni mitungi!”

Joyce anamwomba mama amsaidie
aweze kuona baadhi ya namba.
Mama anaelekeza kidole kwenye
karoti zilizoko bustanini na kuhesabu,
“moja, mbili, tatu, nne.”






Lakini Joyce hana furaha.
“Hizo si namba. Hizo ni karoti!”

Joyce anamwona Linda akihesabu kuku,
anahakikisha kama wote wamerudi nyumbani.






Lakini Joyce hana furaha.
“Hizo si namba. Hao ni kuku!”

Joyce anamwona shangazi akihesabu masaa hadi kufikia muda wa chakula cha usiku.





Lakini Joyce hana furaha.
“Hizo si namba. Hayo ni masaa!”

Joyce haoni namba duniani.
Anaenda kuzungumza na dada yake Maria,
ambaye ana miaka nane na anajua kila kitu.



“Ukitazama kitu chochote kwa usahihi, utaona namba ndani yake,” Maria akasema.

Maria anampa Joyce miwani ya muujiza na kumwambia aende kutafuta namba duniani.







